TANGAZO LA SERIKALI NA. 650 la tarehe 18/11/2022

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI,

(SURA YA 414)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 19 (4))*

NOTISI TAFTISHI KUHUSU MAOMBI YA BEI ZA MAJI YA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MBULU YA MWAKA 2022

Jina

1. Notisi Taftishi Kuhusu Maombi ya Bei za Maji ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mbulu) ya Mwaka 2022.

Tafsiri

2. Katika Notisi hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 414;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa na Sheria ya Mamlaka ua Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka;

"ombi la marekebisho ya bei" maana yake ni ombi la kurekebisha bei za huduma za maji.

"taftishi" inamaanisha mchakato mzima wa kupokea maoni kutoka kwa wadau kuhusu marekebsho ya bei yanayopendekezwa kama inavyooneshwa kwenye Majedwali.

Lengo la taftishi

3. Lengo la taftishi ni kuiwezesha Mamlaka kukusanya maoni ya wadau kuhusu bei zinazopendekezwa.

*Tangazo la Serikali na. 650 (linaendelea)*

Bei zinazopendekezwa

4. Bei zinazopendekezwa na ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mbulu zitakuwa kama zilivyooneshwa kwenye Majedwali ya Notisi hii.

Kushiriki kwenye taftishi

5. Mtu yeyote anayetaka kushiriki kwenye taftishi anaweza kufanya hivyo kwa kuwasilisha maoni kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu kupitia anuani iliyotajwa katika Notisi hii ndani ya siku kumi na nne tangu kuchapishwa katika Gazeti la Serikali kwa Notisi hii.

Pingamizi dhidi ya kuidhinishwa kwa maombi ya bei

6. Mtu yeyote mwenye nia ya kuwasilisha pingamizi dhidi ya kuidhinishwa kwa maombi ya bei atawasilisha pingamizi lake kwa maandishi ndani ya siku tano za kazi tangu siku ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali kwa Notisi hii.

Nakala za maombi

7. Nakala za maombi ya bei ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mbulu zinapatikana kwenye ofisi za Mamlaka saa za kazi kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 10.00 jioni kwa ajili ya taarifa kwa umma na taarifa zaidi zinaweza kupatikana kwa kumwandikia Mkurugenzi Mkuu kupitia anuani iliyotajwa kwenye aya ya 8.

Anuani ya Mamlaka

8. Anuani ya Mamlaka itakuwa:

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji,

Jengo la EWURA,

Kiwanja Na. 3, Kitalu AD,

Medeli Magharibi,

S.L.P. 2857,

Dodoma.

*Tangazo la Serikali na. 650 (linaendelea)*

---

**JEDWALI**

---

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 4*)

**Bei za Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)**

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 540 | 1,500 | 2,000 | 2,000 |
| Taasisi | 550 | 1,500 | 2,000 | 2,000 |
| Biashara | 560 | 1,600 | 2,100 | 2,100 |
| Viwanda | 570 | 1,600 | 2,100 | 2,100 |
| Magati | 500 | 1,400 | 1,900 | 1,900 |

**Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shlingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

**Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kuunganishiwa Huduma (Shilingi kwa Maunganisho)**

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zinazopendekezwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
| Majumbani | 150,000 | Asilimia 20% ya gharama za maunganisho kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 26 ya Kanuni za | | |
| Taasisi | 150,000 | | | |

*Tangazo la Serikali na. 650 (linaendelea)*

| **Kundi la Wateja** | **Ada ya Sasa** | **Ada Zinazopendekezwa** | | |
|---|---|---|---|---|
| | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** | **2024/25** |
| Biashara | 150,000 | Maji za Mwaka 2019 | | |
| Viwanda | 150,000 | | | |

Dodoma, MODESTUS M. LUMATO

1st November, 2022 *Mkurugenzi Mkuu*